ABDULRAHMAN AL-SUMAIT UNIVERSITY(SUMAIT)

جامعة عبد الرحمن السميط

TANGAZO LA KAZI ZA KADA YA AFYA

The Abdulrahman Al-Sumait University (**SUMAIT**) is built on the foundation of the former University College of Education Zanzibar established in 1998 by a charity organization; Kuwait based, **Direct Aid (DA)**. In line with this expansion, SUMAIT wishes to invites applications from suitable **qualified Individuals** to fill the vacant administrative posts as follows:-

1. DAKTARI WA BINAADAM DARAJA LA II (MEDICAL DOCTOR- MD), – (Nasafi Moja)

SIFA ZA MUOMBAJI

- Awe amehitimu Shahada ya Kwanza ya Udaktari wa Binaadamu (Doctor of Medicine)katika chuo kinachotambuliwa na Kamisheni ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU).
- Awe amemaliza mafunzo ya vitendo (Internship) kwa muda wa mwaka mmoja katikahospitali zinazotambuliwa na mabaraza ya Madaktari (MCT na ZMC)
- Awe amesajiliwa na Baraza la Madaktari Zanzibar.

MAJUKUMU

Daktari wa Binaadamu atakuwa na Majukumu haya:-

- Kufanya shughuli zote za utibabu.
- Kusimamia wafanyakazi walio chini yake.
- Kuchunguza, kufatilia na kuzuia miripuko ya magonjwa mbali mbali.
- Kupanga na Kufanya tathmini ya huduma za afya.
- Kuandaa mipango na makisio ya bajeti ya huduma za afya.
- Kutoa huduma za “Outreach Programme”.

2. AFISA TABIBU (CLINICAL OFFICER), Nafasi Mbili (2)

SIFA ZA MUOMBAJI

- **Awe mwenye elimu ya Stashahada ya utabibu (Clinical Medicine) kutoka Chuo**

kinachotambuliwa na serekali.

- **Awe na leseni ya Tabibu Kutoka Baraza la Madaktari Zanzibar.**

MAJUKUMU

1. **Kuchambua na kupanga na kutekeleza huduma za afya ya msingi.**
2. **Kutambua na kutibu mgonjwa wa kawaida.**
3. **Kuweka kumbukumbu za vifaa na zana za kutolea huduma**

3. MPOKEAJI (RECEPTIONNIST), Nafasi Moja (1)

SIFA ZA MUOMBAJI

- Awe amehitimu kidatu cha nne na kuendelea, na kufaulu masomo ya kiengereza, Kiswahili na hisabati na kufuzu mafunzo ya Mapokezi na Upokeaji simu kutoka vyuo vinavyotambuliwa na serekali.
- Awe na uwezo wa kutumia computer na simu janja.

MAJUKUMU

- Kupokea wageni na kuwasaili shida zao.
- Kutunza rejesta ya wageni wa ofisi na kufanya uchambuzi wa wageni wanaoingia ilikutoa ushauri juu ya utaratibu bora wa kupokea wageni.
- Kupokea na kusambaza maombi ya simu za ndani.
- Kutunza na kudumisha usafi wa “Switchboard” na ofisi zake.
- Kuwaelekeza wageni wa ofisi kwa maafisa/ofisi watakakopewa huduma.
- Kupokea simu kutoka nje na kuzisambaza kwa maofisa mbalimbali ofisini.
- Kupokea simu kutoka “Extension” za ndani na kupiga nje ya ofisi.
- Kutunza rejesta ya simu zinazopokelewa kutoka nje ya ofisi na zinazopigwa kwendanje.

4. AFISA MAABARA MSAIDID DARAJA LA III (LAB TECHNICIAN), Nafasi Moja (1)

SIFA ZA MUOMBAJI

- Awe mwenye Stashahada ya kawaida katika fani Maabara (Medical laboratoryTechnician) kutoka Katika Chuo kinachotambuliwa na Serikali.

MAJUKUMU

- Kupima sampuli za maradhi mbali mbali.
- Kutengeneza dawa za kufanyia vipimo vya maabara.
- Kuchukua sampuli za wagonjwa wanaohitaji huduma za maabara.
- Kuhifadhi sampuli mbali mbali zinazotakiwa kufanyiwa uchunguzi.
- Kufanya kazi za ukaguzi wa maabara, vitendanishi, vifaa, kemikali na hifadhi ya kemikali.
- Kuweka kumbukumbu za maabara ambazo zimepatikana wakati wa uchunguzi.

5. AFISA MIONZI MSAIDIZI DARAJA LA III (RADIOLOGY TECHNICIAN), Nafasi Moja (1)

SIFA ZA MUOMBAJI

- Awe mwenye Stashahada ya kawaida katika fani ya Mionzi kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali.
- a na Serikali.

MAJUKUMU

- Kutoa huduma za Mionzi.
- Kusaidia kufundisha wafanyakazi mambo yote yahusianayo na ultrasound.
- Kushiriki katika kutathmini usalama wa wagonjwa kutokana na mashine za ultrasound.

6. MUUGUZI MSAIDIZI DARAJA LA III (NURSING & MIDWIFERY), Nafasi Nne (4)

SIFA ZA WAOMBAJI

- Awe mwenye Stashahada ya kawaida katika fani ya Uuguzi na Ukunga (Nursing and Midwifery) kutoka katika Chuo kinachotambuliwa na serekali.
- Awe amesajiliwa na Baraza la Wauguzi na Ukunga Zanzibar.

MAJUKUMU

- Kutoa huduma za kinga na uzazi.
- Kutambua matatizo ya wagonjwa.
- Kutoa huduma za uuguzi na ukunga kwa wagonjwa.
- Kufanya uchunguzi sahihi wa hali ya Afya ya mgonjwa.
- Kukusanya taarifa muhimu kutoka kwa mgonjwa kuhusu Afya yake.
- Kusimamia usafishaji wa vyombo vya tiba (Sterilization).
- Kutayarisha mpango wa huduma za mgonjwa (Nursing Care Plans) na kuzitekeleza.
- Kutathmini maendeleo ya mgonjwa na kutoa taarifa kwa daktari.

7. MFAMASIA DARAJA LA II (PHARMACIST), Nafasi Moja (1)

SIFA ZA MUOMBAJI

- Awe mwenye Shahada ya Kwanza ya Ufamasia kutoka katika Chuo kinachotambuliwa na Kamisheni ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU).
- Awe amemaliza mafunzo ya mazoezi ya vitendo (internship) ya muda wa mwaka mmoja (1).
- Awe amesajiliwa na Bodi ya Vyakula na Dawa Zanzibar.

MAJUKUMU

- Kuainisha na kutayarisha mahitaji ya mwaka ya dawa na vifaa vyengine vya kitabibu.
- Kutayarisha bajeti kwa ajili ya dawa na vifa vya kitabibu.
- Kufanya manunuzi, kuhifadhi na kuhakiki dawa.
- Kusimamia na kushauri matumizi bora ya dawa.
- Kugawa dawa na vifaa vya kitabibu kwa wagonjwa.
- Kutengeneza na kuchanganya dawa.

8. CLEANER/OEDERLY/HEALTH ATTENDANT, Nafasi Moja (1)

SIFA ZA MWOMBAJI

- Awe amemaliza kidato cha nne na kuendelea.
- Awe na cha kozi ya usafi wa hospital au cheti cha kozi ya usafi, usalama na ushughulikiaji wa taka hatarishi kutoka kwenye taasisi yoyote inayotambulika.

MAJUKUMU

- Kusafisha eneo la hospital, vyumba vya kulaza wagonjwa na maeneo mengine yamatibabu.
- Kushughulikia utupaji wa taka za hospitali.
- Kusafisha vitendea kazi vilivyotumika kugundulia na kutibia magonjwa.
- Kutekeleza majukumu mengine atakayopatiwa na wakuu wake wa kazi.

Mshahara :

Chuo Kikuu cha Abdulrahman Al-Sumait kinatoa Mishahara mizuri pamoja na Marupurupu mengine kwa mujibu wa viwango vya mishahara ya Chuo Kikuu cha Abdulraman Al-Sumait (SUMAIT) na kwa kuzingatia tasnia ya afya.

MASHARTI YA JUMLA KWA KAZI ZOTE:

- Waombaji wote waambatishe cheti cha kuzaliwa.
- Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (**Detailed C.V**) yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (**Referees**) wawili wa kuaminika.
- Maombi yote yaambatane na vyeti vya taaluma, maelezo, nakala za vyeti vya kidato cha nne na kidato cha sita kwa wale waliofikia kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika.
- Postgraduate/Degree/Advanced Diploma/Diploma/Certificates.
- Cheti cha mtihani wa kidato cha IV na VI.
- Computer Certificate.
- Vyeti vya kitaaluma (Professional certificates from respective boards).
- Picha moja “**Passport size**” ya hivi karibuni.

- Testmonials", "Provisional Results", "Statement of results", hati matokeo za kidato cha nne na sita (FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS) HAVITAKUBALIWA.
- Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (TCU na NECTA).

Mwisho wa Maombi:

Maombi yanaweza kuwasilishwa katika Chuo Kikuu cha Abdulrahman Al-Sumait (SUMAIT), Mtaa wa Chukwani, Zanzibar si zaidi ya tarehe iliyotajwa hap ana wakati wa kazi wa not saatisa na nusu **3:30hrs on 30 November 2024**. Or unaweza kuwasilisha maombi yako kupitia katika mtandao wa kielectronic wa:**recruitment@sumait.ac.tz**

Maombi yaelekezwe katika anuwani na uutaratibu huu:

Makamo Mkuu wa Chuo,
Chuo Kikuu cha Abdulrahman Al-Sumait,
S. L. P 1933,
Mtaa wa Chukwani, Zanzibar.
Email: recruitment@sumait.ac.tz